فَضْلُ العَشْرِ من ذِي الْحِجّةِ

FADHILA ZA MASIKU KUMI KATIKA MWEZI WA DHUL-HIJJAH

(MFUNGO TATU)

Mwandishi:

Abu Halima Arafaat Bin Mahmoud

(غَفَرَ اللهُ لَهُ وَلِوَالِدَيْهِ وَلِلْمُسْلِمِيْنَ)

JE TUNAYAPOKEAJE MASIKU KUMI YA DHUL-HIJJAH?

1. TUNAYAPOKEA KWA TOBA:

Muislamu anatakiwa kuipokea misimu yote ya ibada kwa kurudi kwa Allaah kwa kutubia, kwa sababu katika toba kuna kufaulu kwa mja na kupata matakwa yake duniani na akhera, kama alivyosema Allaah Ta'alaa:

﴿وَتُوبُوٓاْ إِلَى ٱللَّهِ جَمِيعًا أَيُّهَ ٱلۡمُؤۡمِنُونَ لَعَلَّكُمۡ تُفۡلِحُونَ﴾

"Na tubuni nyote kwa Allaah, enyi waumini, ili mpate kufaulu"[1].

Amesema Imam Ibn Kathir (Allaah amrehemu):

"فَإِنَّ الفَلَاحَ كُلَّ الفَلَاحِ فِيْ فِعْلِ مَا أَمَرَ اللَّهُ بِهِ وَرَسُولُهُ، وَتَرْكِ مَا نَهَيَا عَنْهُ"

"Hakika kufaulu kote ni katika kufanya aliyo amrisha Allaah na Mtume wake na kuacha waliyoyakataza"[2].

2. KUAZIMIA PAMOJA NA KUJITAHIDI KUFANYA AMALI NJEMA:

Amesema sheikh Ibn Uthaymin رَحِمَهُ اللهُ: "Mtu aliyeswali rakaa mbili katika kumi (la kwanza) la ramadhani na mtu aliyeswali rakaa mbili katika kumi (la kwanza) la Dhul-Hijjah yupi mbora zaidi (katika amali), mtu wa kwanza au wa pili?. (Akasema): mtu wa pili, na jambo hili ni geni kwa watu wa kawaida lakini si geni kwa wasomi (Maulamaa)".

3. KUJIEPUSHA NA AINA ZOTE ZA MAASI:

Kwa sababu Allaah amesema ndani ya Qur'an kuhusu miezi mitukufu:

﴿فَلَا تَظۡلِمُواْ فِيهِنَّ أَنفُسَكُمۡۚ﴾

"Basi msidhulumu humo (katika miezi mitakatifu) nafsi zenu"[3].

1- Surat An-Nuur/31.
2- Tafsiiru Ibn Kathir/Jz.6, Uk.50.
3- Surat Tauba/36

Amesema Imam Ibn Kathir رَحِمَهُ اللهُ:

"أَيْ: فِي هَذِهِ الْأَشْهُرِ الْمُحَرَّمَةِ؛ لِأَنَّهُ آكَدُ وَأَبْلَغُ فِي الْإِثْمِ مِنْ غَيْرِهَا"

"Maana yake: (msidhulumu) ndani ya miezi hii mitakatifu, kwa sababu dhambi hufanywa maradufu zaidi kuliko miezi mingine"(4).

4. KUYAADHIMISHA NA KUYATUKUZA:

Kwa sababu miongoni mwa Taqwa ya mtu ni kutukuza Ibada za Allaah na vitu vyote vitakatifu, kama alivyosema Allaah:

﴿وَمَن يُعَظِّمْ شَعَٰٓئِرَ ٱللَّهِ فَإِنَّهَا مِن تَقْوَى ٱلْقُلُوبِ﴾

"Na anayetukuza Ibada za Allaah, basi hayo ni katika unyenyekevu wa nyoyo"(5).

Kadhalika Allaah anasema:

﴿وَمَن يُعَظِّمْ حُرُمَٰتِ ٱللَّهِ فَهُوَ خَيْرٌ لَّهُۥ عِندَ رَبِّهِۦ﴾

"Na anaye vitukuza vitakatifu vya Allaah, basi hayo ndiyo kheri yake"(6).

HAYA NDIO MASIKU BORA KULIKO SIKU KUMI ZA MWANZO WA MWEZI WOWOTE:

Amesema Mtume ﷺ:

«مَا مِنْ أَيَّامٍ العَمَلُ الصَّالِحُ فِيهِنَّ أَحَبُّ إِلَى اللَّهِ مِنْ هَذِهِ الأَيَّامِ العَشْرِ»

"Hakuna masiku yoyote kufanya amali njema ndani yake kunapendeza zaidi mbele ya Allaah kuliko masiku haya kumi"(7).

4- Tafsiiru Ibn Kathir (Jz. 4, Uk. 148).
5- Surat Al-Hajji/32.
6- Surat Al-Hajji/30.
7- Sunan Tirmidh (757).

Kwa hiyo ni vizuri kwa kila muislamu kujipamba na tabia njema na kufanya mambo mengi ya kheri kadri awezavyo.

Amesema sheikh Ibn Uthaymin رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى :

"وَقَوْلُهُ العَمَلُ الصَّالِحُ يَشْمَلُ الصَّلَاةَ وَالصَّدَقَةَ وَالصِّيَامَ وَالذِّكْرَ وَالتَّكْبِيْرَ وَقِرَاءَةَ القُرْآنِ وَبِرَّ الوَالِدَيْنِ وَصِلَةَ الأَرْحَامِ وَالإِحْسَانَ إِلَى الخَلْقِ وَحُسْنَ الجِوَارِ وَغَيْرَ ذَلِكَ... كُلُّ الأَعْمَالِ الصَّالِحَةِ"

"Na kauli yake (ya kutaja) amali njema, inakusanya Swala, Sadaka, Saumu, Dhikri, Takbiir, Kusoma Qur'an, kuwatendea wema wazazi wawili, Kuunganisha kizazi, Kuwafanyia wema viumbe, Ujirani mwema na yasiyokuwa hayo…. (inaingia) kila amali njema"[8].

Ndio maana watu wema waliotangulia (Salaf) walikuwa wakiyatukuza sana baadhi ya masiku na kuyaadhimisha tafauti na masiku mengine, na miongongoni mwa masiku hayo ni masiku kumi yaa Dhul-Hijjah.

Amesema Abu Uthman An-Nahdi (aliyefariki waka 99H) رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى :

"كَانُوا يُعَظِّمُونَ ثَلاثَ عَشَرَاتٍ: الْعَشْرَ الأُوَلَ مِنْ ذِي الْحِجَّةِ، وَالْعَشْرَ الأَخِيرَ مِنْ رَمَضَانَ، وَالْعَشْرَ الأُوَلَ مِنَ الْمُحَرَّمِ"

"Walikuwa (Maswahaba) wanayatukuza makumi matatu, kumi la mwanzo wa Dhul-Hijjah, kumi za mwisho la ramadhani, na kumi la mwanzo wa Muharram"[9].

FADHILA ZA MASIKU KUMI YA DHUL-HIJJAH (MFUNGO TATU):

1. ALLAAH AMEAPIA KWA MASIKU HAYA KUMI:

Allaah ameapa kwa masiku haya kumi, na hiyo ni ishara ya kwamba hayo ni masiku matakatifu, kwa sababu yeye Allaah ni mtukufu kwa hiyo hawezi kuapia isipokuwa kwa kitu kitukufu.

8- Sharhu Riyyadhis Swaalihin (Jz.6, Uk. 113). Ibn Uthaymin.
9- At-Tabswira (Jz. 2, Uk. 124). Cha Ibnul Jauzi (rahimahullaah).

Allaah anasema:

﴿وَٱلۡفَجۡرِ ** وَلَيَالٍ عَشۡرٍ﴾

“Naapa kwa alfajri ** Na masiku kumi ya mwezi wa Dhul-Hijjah”[10].

Amesema Imam Ibn Kathir رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى:

"الْمُرَادُ بِهَا عَشْرُ ذِي الْحِجَّةِ. كَمَا قَالَهُ ابْنُ عَبَّاسٍ، وَابْنُ الزُّبَيْرِ، وَمُجَاهِدٌ، وَغَيْرُ وَاحِدٍ مِنَ السَّلَفِ وَالْخَلَفِ"

“Makusudio ya masiku hayo ni siku kumi za mwanzo wa Dhul-hijjah. Kama alivyosema Ibn Abbas, Ibn Zzubeir, Mujahid, na wengi katika wanachuoni wa Salaf na Khalaf (waliofuatia)”[11].

2. HAYO NDIO MASIKU BORA YA DUNIA:

Mtume ﷺ amebainisha kwamba haya ndio masiku bora zaidi duniani:

"أَفْضَلُ أَيَّامِ الدُّنْيَا أَيَّامُ الْعَشْرِ"

“Masiku bora ya duniani ni siku kumi (za mwanzo wa Dhul-hijjah”[12].

3. NDANI YAKE KUNA SIKU YA ARAFA:

Katika masiku kumi hayo kuna siku ya Arafa (siku wanayosimama mahujaji wote katika viwanja vya Arafaat) katika maeneo matakatifu huko Makka.

- Siku hiyo watu wengi huachwa huru na moto:

"مَا مِنْ يَوْمٍ أَكْثَرَ مِنْ أَنْ يُعْتِقَ اللهُ فِيهِ عَبْدًا مِنَ النَّارِ، مِنْ يَوْمِ عَرَفَةَ"

“Hakuna siku yoyote ambayo Allaah anakithirisha zaidi kumuacha mja huru na moto kuliko siku ya Arafa”[13].

10- Surat Al-fajri/1-2.
11- Tafriiru Ibn Kathir (Jz. 8, Uk. 390).
12- Sahihil Jaami’ (2013).
13- Sahihi Muslim (436).

- Dua bora ni dua iliyoombwa siku hiyo ya Arafa:

"خَيْرُ الدُّعَاءِ دُعَاءُ يَوْمِ عَرَفَةَ"

“Dua bora ni dua ya siku ya Arafa”[14].

- Funga ya siku ya Arafa inafuta madhambi ya miaka miwili:

Mtume ﷺ aliulizwa kuhusiana na funga ya siku ya Arafa, akasema:

«يُكَفِّرُ السَّنَةَ الْمَاضِيَةَ وَالْبَاقِيَةَ»

“Inafuta madhambi ya mwaka uliopita na (mwaka) unaokuja”[15].

4. NDANI YAKE KUNA SIKU KUBWA, NAYO NI SIKU YA EID YA KUCHINJA:

Miongoni mwa siku tukufu mbele ya Allaah Ta’alaa ni siku hii ya Eid.

Amesema Mtume ﷺ:

«إِنَّ أَعْظَمَ الْأَيَّامِ عِنْدَ اللَّهِ يَوْمُ النَّحْرِ ثُمَّ يَوْمُ الْقَرِّ»

“Hakika siku kubwa mbele ya Allaah ni siku ya (Eid ya) kuchinja kisha siku ya Qarri”[16].

Yaumul Qarri (siku ya kutulizana Minaa) ni siku inayofuata baada ya siku ya Eid (tarehe 11), na imeitwa kwa jina hilo kwa sababu Mahuaji wote siku hiyo wanakuwa wametulizana huko Minaa, kwa hiyo siku hiyo pia ni miongoni mwa masiku matukufu.

5. NDANI YAKE HUKUSANYIKA IBADA MBALIMBALI KUBWA:

Amesema Ibn Hajar رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى:

"وَالَّذِي يَظْهَرُ أَنَّ السَّبَبَ فِي امْتِيَازِ عَشْرِ ذِي الْحِجَّةِ لِمَكَانِ اجْتِمَاعِ أُمَّهَاتِ الْعِبَادَةِ فِيهِ وَهِيَ الصَّلَاةُ وَالصِّيَامُ وَالصَّدَقَةُ وَالْحَجُّ وَلَا يَتَأَتَّى ذَلِكَ فِي غَيْرِهِ"

14- Sunan Tirmidh (3585).
15- Sahihi Muslim (197).
16- Mishkaatul maswaabih (Jz. 2, Uk. 810) hadithi namba (3643).

“Na lenye kudhihiri ni kwamba kutukuzwa siku kumi za Dhul-Hijjah ni kwa sababu ndio mahali pa mkusanyiko wa ibada mbalimbali kubwa, ambazo ni Swala, Funga (saumu), Sadaka na Hija, na wala halipatikani hilo katika siku kumi nyingine zisizokuwa hizi”[17].

6. KUYATUKUZA MASIKU HAYO NI KUJIFANANISHA NA MAHUJAJI:

Si kila mtu ana uwezo wa kwenda Makka kutekeleza ibada ya hija, lakini Allaah ameweka ibada bora kwa yule ambaye hakwenda.

Amesema Ibn Hajar رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى:

"لَمَّا كَانَ اللهُ سُبْحَانَهُ وَتَعَالَى قَدْ وَضَعَ فِيْ نُفُوْسِ المُؤْمِنِيْنَ حَنِيْنًا إِلَى مُشَاهَدَةِ بَيْتِهِ الحَرَامِ وَلَيْسَ كُلُّ أَحَدٍ قَادِرًا عَلَى مُشَاهَدَتِهِ فِيْ كُلِّ عَامٍ فَرَضَ عَلَى المُسْتَطِيْعِ الحَجَّ مَرَّةً وَاحِدَةً فِيْ عُمُرِهِ وَجَعَلَ مَوْسِمَ العَشْرِ مُشْتَرَكًا بَيْنَ السَّائِرِيْنَ وَالقَاعِدِيْنَ فَمَنْ عَجَزَ عَنِ الحَجِّ فِيْ عَامٍ قَدَرَ فِي العَشْرِ عَلَى عَمَلٍ يَعْمَلُهُ فِيْ بَيْتِهِ يَكُوْنُ أَفْضَلَ مِن الجِهَادِ الَّذِيْ هُوَ أَفْضَلُ مِن الحَجِّ"

“Wakati Allaah Ta’alaa ailipoweka ndani ya mioyo ya waumini shauku/hamu ya kuiona Nyumba yake Takatifu (Al-K’ba), na hali ya kuwa sio kila mtu anaweza kuiona kila mwaka, akafaradhisha juu ya mwenye uwezo kuhiji mara moja tu katika uhai wake, na akaujalia msimu wa masiku kumi (Dhul-Hijjah) ni (msimu) wa kushirikiana baina ya wasafiri (walioenda Makka) na ambao hawakwenda, basi yeyote asiyeweza kuhiji katika mwaka ana uwezo katika siku kumi hizi kufanya amali akiwa nyumbani kwake, (amali) ambayo ni bora kuliko (kupigana) Jihad ambayo ni bora kuliko ibada ya Hijja”[18].

Abu Halima Arafaat

Pongwe Tanga

29/Dhul qa’da/1443H – 29/06/2022M.

[17]- Fat-hul baari (Jz. 2, Uk. 460).

[18]- Latwaaiful Ma’arif (272).